

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA**

**22 MEI, 2024**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

KIKAO CHA THELATHINI NA MOJA TAREHE 22 MEI, 2024

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**III. MASWALI:**

**OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**405. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itapeleka fedha za kuendeleza ujenzi wa Zahanati ya Mtego wa Simba katika Halmashauri ya Wilaya ya Morogoro.

**406. MHESHIMIWA DEO KASENYENDA SANGA (MAKAMBAKO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Stendi ya Mabasi na Soko Kuu Makambako Mjini kupitia Mradi wa Kuboresha Miji 45 nchini.

**WIZARA YA NISHATI:**

**407. MHESHIMIWA ANATROPIA LWEHIKILA THEONEST (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, lini Vijiji na Vitongoji vyote vya Wilaya ya Kyerwa vitafikiwa na umeme.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**408. MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, lini Serikali italetwa Muswada wa Sheria ya Ndoa ili iendane sambamba na vita dhidi ya ndoa za utotoni.

**409. MHESHIMIWA ESTHER EDWIN MALLEKO (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, upi mkakati wa Serikali kuimarisha huduma za usuluhishi kwa migogoro ya ndoa na matumizi ya Watoto.

**410. MHESHIMIWA ABUBAKAR DAMIAN ASENGA (KILOMBERO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali inaona bado kuna umuhimu wa Sheria ya *Plea – Bargaining*.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**411. MHESHIMIWA STELA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, Serikali imefikia hatua gani kutoa Mikopo ya Elimu ya Juu na ya Kati kama ruzuku kwa Watu wenye Ulemavu.

## **WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

### **412. MHESHIMIWA TOUFIQ SALIM TURKY (MPENDAE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:-

Je, lini katazo la Bodi ya Nyama Tanzania la kuzuia matumizi ya magogo kukatia nyama litafanyiwa kazi ili kuwanusuru Watanzania kupata athari za kiafya.

## **WIZARA YA UJENZI:**

### **413. MHESHIMIWA JOSEPHINE TABITHA CHAGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itajenga Barabara ya kutoka Busisi kupitia Buyagu – Nyang’hwale hadi Kahama kwa kiwango cha lami.

### **414. MHESHIMIWA DKT. DAVID MATHAYO DAVID (SAME MAGHARIBI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Barabara ya Mwembe – Mbaga hadi Mamba itafanyiwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha Lami.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **415. MHESHIMIWA NASHON WILLIAM BIDYANGUZE (KIGOMA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itapeleka fedha kukarabati Skimu ya Umwagiliaji ya Kalya na Mgambazi - Uvinza.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

*(Majadiliano yanaendelea)*

**DODOMA  
22 MEI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**